JIPYA

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

TANGAZO

## UKUSANYAJI WA USHURU WA MAPATO KWENYE VYOO VYA STENDI KUU YA MABASI, SOKO KUU NA SOKO LA SABASABA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**ZABUNI NA. LGA-053/2020/2021/HQ/NS/10**

## MWALIKO WA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi inatangaza zabuni za ukusanyaji wa mapato katika vyoo vya **Stendi kuu ya mabasi, Soko kuu na Soko la Sabasaba** kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Juni, 2021.

**<u>MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI</u>:**

- Mwombaji lazima awe na ofisi inayotambulika, anuani ya posta na namba ya simu.
- Mwombaji awe na Leseni hai ya Biashara ya aina ya zabuni anayoomba, TIN namba pamoja na nyaraka nyingine muhimu.
- Mwombaji anatakiwa kuambatanisha taarifa ya Benki (Bank statement) ya mwaka mmoja hadi 30/04/2020 ili kuthibitisha uwezo wake kifedha.
- Mwombaji wa zabuni ya kukusanya ushuru / mapato ataje kiasi atakachokusanya kutoka chanzo husika na kuilipa Halmashauri. (Mzabuni atalipwa asilimia ishirini (20%) ya makusanyo kwa kila mwezi.
- Ada ya Tshs. 50,000/= kwa mzabuni ilipwe katika akaunti ya makusanyo ya ndani ya Manispaa. Mzabuni atapaswa kuambatanisha stakabadhi ya malipo wakati wa kuwasilisha zabuni yake.
- Mwombaji anatakiwa aambatanishe uzoefu wake katika ukusanyaji mapato ya Umma
- Halmashauri ya manispaa ya Lindi haitalazimika kukubali zabuni ya chini kabisa au ya juu.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI HAYO:**

Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa kwenye bahasha na kuwekwa lakiri (seal). Juu ya bahasha iandikwe namba ya zabuni, na itumwe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu, Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
S. L. P 1070
**LINDI**

Zabuni zinaweza kupelekwa kwa mkono au posta na siku ya mwisho kupokea zabuni hizo ni siku ya Jumatatu tarehe 11/06/2020 saa 4.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo katika Ofisi ya Kiengo cha Manunuzi na Ugavi muda mfupi baada ya zabuni kupokelewa mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaopenda

Wote mnakaribishwa.

Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
**LINDI**

MKURUGENZI WA MANISPAA
LINDI

28/5/2020